## Wizara ya Kazi ya Marekani

## Matokeo ya  Mwaka 2021 kuhusu Aina Mbaya zaidi za Utumikishwaji wa Kazi kwa Watoto

# Tanzania

Mnamo mwaka 2021, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maendeleo kiasi katika juhudi za kutokomeza aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa kazi kwa watoto. Serikali ilitoa waraka ikiagiza kwamba wasichana waweze kurudi shuleni baada ya kumaliza ujauzito wao, na kubatilisha uungaji mkono wake wa awali wa kuwafukuza kabisa wasichana waliokuwa wamepata mimba. Serikali pia iliahidi rasilimali za ziada za kushughulikia vikwazo vingine kwa upatikanaji wa elimu, ikiwa ni pamoja na utoaji wa madarasa na vyoo vya ziada, pamoja na madawati. Zaidi ya hayo, serikali iliwezesha kampeni za uhamasishaji kuhusiana na biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu na ilitoa mafunzo kwa kamati 17 za mitaa zinazolenga ajira kwa watoto na masuala mengine yanayohusiana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Hata hivyo, watoto nchini Tanzania hutumikishwa kwa kazi zilizo mbaya zaidi kwa watoto, ikiwa ni pamoja na kutumikishwa katika uchimbaji madini, uchimbaji mawe na kazi za majumbani. Watoto pia hufanya kazi hatarishi katika kilimo. Serikali ya Bara haikutoa habari hadharani kuhusu juhudi zake za utekelezaji wa sheria za kazi na ile ya jinai. Mapengo mengine yamebaki katika mfumo wa kisheria na utekelezaji wa sheria zinazohusu ajira kwa mtoto, ikiwa ni pamoja na kinga kwa utumiaji wa watoto katika shughuli haramu na kazi za majumbani na uwezekano wa upungufu wa idadi ya wakaguzi wa kazi kulingana na ukubwa wa nguvu kazi ya Tanzania.

**Jedwali 11. Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Kazi kwa Watoto**

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| Mfumo wa Kisheria | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba ulinzi wa umri wa kima cha chini unatumika kwa watoto wote, wakiwemo wale wanaofanya kazi za majumbani. | 2013 – 2021 |
| | Bara | Panua orodha ya kazi na shughuli hatarishi zilizopigwa marufuku kwa watoto ili kuhakikisha kwamba orodha hiyo inajumuisha kupalilia na usindikaji kwenye uzalishaji wa tumbaku, karafuu, kahawa, katani, na chai. | 2016 – 2021 |
| | Bara | Haramisha matumizi ya watoto katika shughuli haramu, hususani katika kuzalisha na kuuza madawa ya kulevya. | 2012 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Haramisha uajiri wa watoto chini ya umri wa miaka 18 unaofanywa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali. | 2016 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Weka kwa mujibu wa sheria, umri wa lazima kwa elimu ambao ni sawa au zaidi ya umri wa chini wa kufanya kazi. | 2017 – 2021 |

**Jedwali 11. Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Kazi kwa Watoto**

| Eneo | Chombo Husika | Hatua Iliyopendekezwa | Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa |
|---|---|---|---|
| | Bara | Weka kwa mujibu wa sheria, elimu ya bure ya msingi kwa umma. | 2016 – 2021 |
| Utekelezaji | Bara | Weka utaratibu wa kutathmini adhabu za kiraia za ukiukaji wa utumikishwaji wa kazi kwa watoto. | 2017 – 2021 |
| | Zanzibar | Rasimisha mafunzo ya wakaguzi wa kazi, ikiwemo kuwapatia mafunzo wakaguzi wapya wa kazi mwanzoni mwa ajira zao na pia kozi za mafunzo ya ziada. | 2019 – 2021 |
| | Bara | Chapisha habari kuhusu juhudi za utekelezaji wa sheria za kazi. | 2011 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Hakikisha uteuzi wa afisa wa kazi mwenye kujituma kwa dhati kwenye kila mkoa, na chapisha habari hiyo. | 2013 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Ongeza idadi ya wakaguzi wa kazi ili kukidhi ushauri wa kiufundi wa ILO. | 2013 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Toa ufadhili wa kutosha ili kuhakikisha utekelezaji wa kutosha wa sheria za kazi. | 2013 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba utaratibu wa malalamiko ya utumikishwaji wa kazi kwa watoto una rasilimali za kutosha za kutekeleza operesheni. | 2021 |
| | Zanzibar | Rasimisha mafunzo ya wachunguzi wa utekelezaji wa sheria za makosa ya jinai, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo wachunguzi wapya. | 2019 – 2021 |
| | Bara | Chapisha habari juu ya juhudi za utekelezaji wa sheria ya jinai zinazohusiana na aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa kazi kwa watoto. | 2012 – 2021 |
| | Zanzibar | Chapisha habari kuhusu juhudi za utekelezaji wa sheria za jinai zinazohusiana na aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa kazi kwa watoto, ikiwa ni pamoja na mafunzo, idadi ya uchunguzi, na adhabu zilizotolewa kwa ukiukaji unaohusiana na aina mbaya zaidi za utumikishwaji wa kazi kwa watoto. | 2021 |
| Uratibu | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba kamati za uratibu zinafanya kazi na zina uwezo wa kutekeleza mamlaka yaliyokusudiwa. | 2018 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu na pia vyombo vingine | 2021 |

| Jedwali 11. Hatua Zilizopendekezwa za Serikali Kutokomeza Utumikishwaji wa Kazi kwa Watoto | | | |
|---|---|---|---|
| **Eneo** | **Chombo Husika** | **Hatua Iliyopendekezwa** | **Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa** |
| | | vya uratibu vina rasilimali za kutosha ili kutekeleza mamlaka zao. | |
| Sera za Serikali | Bara na Zanzibar | Hakikisha kwamba shughuli zinafanywa ili kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza utumikishwaji wa kazi kwa Watoto na pia kuchapisha matokeo ya shughuli zinazotekelezwa katika kipindi cha kuripoti. | 2020 – 2021 |
| | Bara | Ondoa masharti katika Mtihani wa Kumaliza Masomo ya Shule ya Msingi ambayo ni vizuizi kwa elimu, kama vile sera ya kutorudia mtihani. | 2016 – 2021 |
| | Zanzibar | Jumuisha mikakati ya kuzuia na kutokomeza utumikishwaji wa kazi kwa watoto na pia hakikisha utekelezaji kamili wa Sera ya Elimu Zanzibar ili kupunguza idadi ya wanaoacha masomo. | 2018 – 2021 |
| Mipango ya Kijamii | Bara | Hakikisha upatikanaji wa elimu kwa wasichana walioondolewa shuleni wakati wa ujauzito. | 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Imarisha juhudi za kuondoa vizuizi na pia fanya elimu ipatikane kwa watoto wote nchini Tanzania kwa kuhakikisha rasilimali za kutosha kwa watoto wenye ulemavu na matatizo ya kujifunza, kuongeza rasilimali kwa walimu, vyumba vya madarasa, chakula, na vifaa vya usafi wa mazingira, huku ikiepukwa kuzilipisha familia gharama zisizo rasmi, ikiwa ni pamoja na sare za shule, vitabu, na vifaa vingine vya kujifunzia. | 2010 – 2021 |
| | Bara | Ondoa vizuizi vya kisheria vinavyopunguza kusambaziana habari inayohusu utumikishwaji wa kazi kwa mtoto. | 2020 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Boresha upatanishaji wa hatua za kuzuia na kutokomeza ajira kwa watoto na kuziingiza hatua hizo katika Mpango wa Mfuko wa Kijamii wa Uhamishaji wa Fedha Taslimu wenye Masharti ili kuongeza ufanisi wake katika kuzuia na kutokomeza utumikishwaji wa kazi kwa watoto. | 2020 – 2021 |
| | Bara na Zanzibar | Unganisha mipango inayojumuisha kilimo, ujenzi, huduma za majumbani, uvuvi, na sekta zisizo rasmi ili kushughulikia watoto wanaohusishwa katika utumikishwaji wa kazi kwa watoto. | 2017 – 2021 |